

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA MADARASA, MABWENI NA VYOO
KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017**

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa ndugu Amour Hamad Amour, mbele yako ni mradi wa ujenzi wa madarasa manne sambamba na ujenzi wa mabweni mawili, ujenzi wa vyoo matundu 14 na ukarabati wa bwalo la chakula na bweni moja ambayo ni miradi inayotekelezwa katika shule hii. Miradi hii kwa pamoja ina thamani ya Tshs. **264,157,189.00**. Kati ya hizo, Tshs. **259,000,000.00** ni fedha kutoka fungu la lipa kwa matokeo (P4R) Tsh. na Tsh. **5,157,189.00** ni mapato ya ndani ya Halmashauri. Fedha hii inafanya kazi kama ifuatavyo:-

- (i) 80,000,000/= Ujenzi wa Madarasa manne (4) na samani zake
- (ii) 150,000,000/= Ujenzi wa Mabweni mawili na utengenezaji wa vitanda 128
- (iii) 16,157,189/= Ujenzi wa vyoo matundu 14
- (iv) 18,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa jiko, Bwalo na Bweni moja

Kulingana na adhima ya Serikali ya kuwawezesha Vijana kujitegemea kiuchumi na kukuza pato la familia pamoja na kuwajengea uwezo wa kujitegemea, Halmashauri imetoa kipaumbele kwa vijana kufanya kazi zote za Ujenzi na ukarabati wa shule. Tunavyo vikundi vine vilivyosajiliwa na Halmashauri yetu na ndivyo vinavyofanya kazi ya ujenzi kwenye Miradi. Vikundi hivyo ni:

1. Lugongwe “Construction group” lenye vijana wenye fani ya Ujenzi, Ufundi Umeme, Mafundi bomba na Uselemala. Jumla vijana 28
 2. Umoja ni nguvu, lenye vijana wa fani ya Ujenzi na fundi Bomba. Jumla vijana 22
 3. Mnondo group lenye vijana wa fani za Ufundi Ujenzi, Umeme na Mafundi bomba. Jumla vijana 12
 4. Mkela group lenye Vijana wenye fani za Ujenzi na Uselemala. Jumla vijana 10.
- Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge, tunakuomba utuwekee jiwe la msingi katika mradi huu.

“Mwenge Oyee”.

.....
HILLARY BASA NGELA
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI UTETE